# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

Aprili 2017

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika".
- Joseph Wresinski (1917–1988) founder of ATD Fourth World -

ATD FOURTH WORLD

## Tahariri



Wapendwa marafiki,

Ni tumaini langu kwamba nyote hamjambo. Katika chapisho hili ninayo furaha kuwaleteeni habari za mafanikio kuhusu shule za msingi, mkutano mkuu wa Dakar, Senegal na kampeni ya uhamasishji ya ATD 2017.

Ninao uhakika kwamba mnakumbuka chapisho la mwezi wa July 2016, tulipotoa mapendekezo kumi na matano yaliyotokana na utafiti wa shule za msingi uliofanywa na wanachama wa ATD katika wilaya ya Kinondoni. Wanachama hao hao wakiwemo watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri, walimu na wafanyakazi wa kujitolea wa ATD, sasa wanafanya kazi ya kutetea mapendekezo hayo kwa wadau mbali mbali wa elimu, wazazi, viongozi wa serikali za mitaa na NGO zinazofanya kazi katika sekta ya elimu. Katika mikutano mitatu ya wazazi na walimu iliyofanyika katika shule za msingi msingi Pwani, Tandale na Melenia ya tatu washiriki zaidi ya 1,400 walihudhuria, mapendekezo yalipokelewa vizuri na kusababisha mijadala yenye shauku kubwa kati ya walimu, wazazi,na kamati za shule. Kazi hii ya kutetea matokeo ya mapendekezo itaendelea katika mwaka wote wa 2017.

Chapisho hili linalenga hasa kukuletea kisa cha utashi wa familia moja katika kuzishinda changamoto na kutengeneza ushirikiano mpya uliojengwa katika uelewa na heshima, ukionesha jinsi mapendekezo ya Elimu kwa Wote yanavyoweza kuleta msukumo kwa uhalisia katika familia moja. Tangu 2016 hadi 2017 mchakato wa Mkutano Mkuu umekuwa ukifutiliwa katika kanda ya Afrika, ukuhusisha 34 ya wanachama wa ATD. Mkusanyiko wa Dakar mwanzoni mwa mwezi March ulikuwa matokeo ya huu mchakato.

Ukurasa wa mwisho umetolewa kwa kumbukumbu ya miaka mia moja ya kuzaliwa muasisi wa shirika la ATD Joseph Wresinski; miaka sitini ya kuanzishwa kwa shirika 1957 na miaka thelathini tangu siku ya Kutokomeza Umaskini Duniani ilipoadhimishwa mara ya kwanza tarehe 17 Oktoba 1987. Katika mwaka huu maalumu wanachama wa ATD watajitoa kikamilifu katika tamko la UMASKINI BASI: Wakiwepo watu kutoka duniani kote kuchukua hatua katika kuutokomeza umaskini,

Robert Jordan,
Timu ya Uongozi, ATD Dunia ya Nne, Tanzania.




***"Mara nyingi nilikuwa nikifikiria nini kitatokea kwa watoto wangu kesho"***
Hadithi ya matumaini kwa familia zote kuhusu watoto wawili ambao walikuwa hawaendi shule na kuweza kuvishinda vikwazo………………………………………………..**Ukurasa 2**

***"Kutokana na kisa hiki cha mafanikio kuhusiana na mahudhurio ya shule ya msingi tunaweza kujifunza kitu gani?"***
Ni vipi hadithi za matumaini zinavotupa mapendekezo yenye uhalisia……………………………………………………**Ukurasa 4**

***"Dakar 2017: jitolee kwa moyo wako wote bila kumuacha mtu nyuma."***
Jinsi gani ya kusaidia katika kujitolea kwetu? Habari kutoka mkutano wa kimataifa na wanachama wa ATD Dunia ya Nne. **Ukurasa 6**

***"Siku maalumu ya kuadhimmisha miaka 100 ya kuzaliwa Joseph Wresinski, muasisi wa ATD Dunia ya Nne."***
Matukio kupitia picha……………………………………**Ukurasa 8**

# "Mara nyingi nilikuwa nikifikiria nini kitatokea kwa watoto wangu kesho"

Kwa watoto wanaopambana na ugumu wa maisha ya umaskini uliokithiri kila siku, kuishi karibu na shule hakuna maana ya uhakika wa kwenda shule. Bado vikwazo vinaweza kuwepo, kama vile kutokuwa na ufahamu wa mfumo wa kuhamisha wanafunzi – au kuhusu maamuzi kama vile uoga wa kuzungumza na watu walio katika mamlaka. Vikwazo hivi vinaweza kuwa vingi na vigumu.

Leo tunawaleteeni kisa kinachohusu watoto wawili waliokosa nafasi ya kusoma shule ya msingi kwa sababu ya vizingiti halisi vya maisha. Hata hivyo, uwepo wa utashi, kusindikizwa kwa karibu na ushirikiano mpya, viliweza kushinda vizingiti na sasa watoto hawa wanafurahi kwenda shule.

Kisa chetu kinamhusu mama R. mzazi pekee na wanaye watatu. Kisa kinaanzia wakati mabinti zake wadogo walipokuwa na umri wa miaka 11 na 9, mwanaye wa kiume akiwa na miaka minne. Familia hii inaishi kaskazini mwa Dar es salaam karibu na machimbo ya kokoto. Maisha kwao hayakuwa imara kabisa, mama anafanya kazi ya kuvunja kokoto kwa ajili ya kipato cha matumizi ya familia. Anakabiliwa na tatizo la shinikizo la damu na pia matatizo ya moyo. Hii ina maana kwamba hawezi kufanya kazi katika baadhi ya siku hali inayoongeza matatizo katika familia. Matatizo ya afya yake humletea wasiwasi mkubwa, hususani anapokabiliana na maafisa kama vile wa afya, viongozi wa serikali za mitaa na walimu.

Familia ilikuwa imehamia kutoka wilaya nyingine kwa takribani mwaka mmoja nyuma. Kabla ya kuhamia watoto wakubwa wawili walikuwa wanahudhuria katika shule ya msingi, lakini walipohama mama yao alikuwa hajui utaratibu wa kufuatilia uhamisho. Alikuwa amejaribu, lakini kwa kuwa alikuwa hajui kusoma wala kuandika, baada ya majaribio kadhaa alikata tamaa na kuacha. Ilimhuzunisha sana kuwaona watoto wake wakibaki nyumbani. Alituambia, "Mara zote nilifikiria kitakachowatokea wanangu kesho".

Hatimaye mama R. alikutana na rafiki wa ATD, mwanaharakati ambaye alikuwa anasaidia katika darasa la watu wazima katika jumuiya ile. Alimshawishi mama R. kujiunga na darasa na kuifahamu ATD, ushauri ambao aliutekeleza. Mama R. alikutana na wafanyakazi wa kujitolea wa ATD waliokuwa wakifanya kazi katika jumuiya yake kupitia mradi wa elimu ya watu wazima na mradi wa vyeti vya kuzaliwa. Wafanyakazi wa kwanza wa kujitolea walipomtembelea waliwaona watoto wake wakubwa wakiwa nyumbani. Wakihofia kumfedhehesha, waliepuka kumuuliza lolote kuhusiana na hali hiyo. Waliendelea kumtembelea na siku moja mama R. Alipata ujasiri na kuwaamini na kuzungumzia suala hilo. Baada ya kuitembelea familia kwa wiki kadhaa ilijidhihirisha wazi kwamba msaada aliokuwa anahitaji ulikuwa kumsindikiza kupata nafasi ya shule kwa ajili ya mabinti zake wadogo wawili.

Fursa mbili zilikuwa: kufuatana na mama ili kupata fomu za uhamisho katika shule ya awali kuwahamishia katika shule mpya, au kuwatafutia nafasi katika darasa la Memkwa ambalo hupokea watoto waliokaa nje ya shule kwa muda mrefu. Mama alipendekeza darasa la Memkwa.

Kwa kuwa wafanyakazi wa kujitolea wa ATD walikuwa wanazifahamu baadhi ya shule katiika eneo hilo, ambazo hazikuwa mbali kutoka katika makazi ya familia, walikubaliana kufuatana na mama R. pamoja na mabinti zake wawili kukutana na mwalimu mkuu **(1)**. Hapo waliarifiwa kwamba darasa la Memkwa lilikuwepo lakini walishauriwa kuzungumza na mwalimu wa darasa kuangalia endapo kulikuwa na nafasi. Huu mkutano wa kwanza na mwalimu wa darasa ulimfedhehesha sana mama kwa kuwa mwalimu alimshutumu - mbele ya wanaye – kwa kutowajali wanaye na kuwabakiza nyumbani kwa muda mrefu hivyo. Wafanyakazi wa kujitolea wa ATD walisema hiyo haikuwa njia nzuri ya kumwambia mama, tupo hapa kwa ajili ya kutafuta nafasi katika shule, na waliamua kuondoka, wakitarajia kurejea tena siku ya pili kuzungumza na mwalimu mkuu. Baada ya kuondoka pale shuleni ilichukua muda mrefu na maneno ya faraja kuweza kufanya mama atulie.

***"Nini utakuwa mustakabali wa nchi yetu iwapo tutawafukuza watoto hawa. Iwapo hawatapata nafasi ya kwenda shule, watakosa fursa ya kuwa mtu mashuhuri katika jumuiya yetu,kama vile mwalimu, polisi, au kiongozi wa serikali ya mtaa. Wakipata nafasi hii ya kusoma,nchi yetu itakuwa salama siku zijazo".***

Siku iliyofuata mfanyakazi mmoja wa kujitolea wa ATD, akiwa peke yake, alimtembelea mwalimu mkuu akamsimulia matukio ya siku iliyopita walipokutana na mwalimu wa Memkwa. Mwalimu mkuu alisikiliza na alimwonea huruma yule mama na kusikitishwa kwa kitendo cha mwalimu. Alimwambia yule mfanyakazi kumleta mama pamoja na wanaye siku iliyofuata waweze kuanza shule **(2)**. Kesho yake, mama R. akifuatana na mfanyakazi wakujitolea wa ATD waliwaleta watoto shuleni, wakaanza rasmi masomo katika darasa la Memkwa.

Kwa watoto ambao waliosimama kwenda shule kwa zaidi ya mwaka mmoja, kurudi tena shule wanahitaji msaada wa karibu wa kuongozana nao na kufikia malengo. Watoto wanahitaji kukabiliana na utaratibu, muundo na kanuni za shule tena, na watoto wakubwa ambao waliokuwa mitaani kwa kipindi fulani, hii inaweza kuwa ni changamoto kubwa.

Muda si mrefu baada ya kuanza shule, wasichana wale wadogo wawili wa mama R. pamoja na rafiki yao walitoroka shule na kwenda kucheza muda wa masomo. Polisi jamii aliwakamata na kuwapeleka shuleni. Mwalimu mkuu alistuka kuwaona wakiwa wamesindikizwa na polisi jamii hivyo akawafukuza wote.

Mama R. alikwenda shuleni kuwaombea kwa mwalimu mkuu ili aweze kuwafikiria tena bila mafanikio. Mwalimu mkuu hakumkubalia. Akiwa amedhalilika na kufadhaika, aliwaendea marafiki wa ATD na kuwaomba wamsaidie na wafuatane naye tena.

Mfanyakazi wa kujitolea alikwenda shuleni kuangalia kinachoweza kufanyika. Hapo alikutana uso kwa uso na mwalimu mkuu, mwalimu wa darasa la Memkwa, polisi na mwenyekiti wa kamati ya shule. Wote kwa pamoja walipinga suala la watoto kurejeshwa mwalimu mkuu akisisitiza kwamba kuhusika kwa polisi kuwarejesha watoto shuleni ilikuwa ni aibu kwa shule yake. Hatimaye alipopewa fursa ya kuzungumza mfanyakazi wa kujitolea wa ATD alihoji, “Mustakabali wa nchi yetu utakuwaje endapo tutawafukuza hawa? Endapo hawatapata nafasi ya kwenda shule watakosa fursa ya kuwa watu mashuhuri katika jamii yetu, kama vile walimu, polisi au viongozi wa serikali za mitaa. Wakipata fursa hii ya kusoma nchi yetu itakuwa salama siku zijazo”. Baada ya ushawishi mkubwa, mfanyakazi wa kujitolea wa ATD akichukua jukumu la kutetea haki za hawa watoto wawili. Mwalimu mkuu alikubali warejee tena shuleni.

Tangu hapo ilikuwa muhimu kuwasaidia kwa karibu zaidi. Mkuu wa shule, mwalimu wa Memkwa na mama walikubaliana kupeana namba za simu hivyo wakawa katika mawasiliano ya mara kwa mara. Kwa kipindi maalumu mfanyakazi wa ATD alifuatana na mama kwenda shuleni kufuatilia maendeleo ya hawa mabinti zake wawili. Hatimaye mama aliweza kuchukua jukumu hili yeye mwenyewe **(3)**. Mama R. alifahamika shuleni na walimu nao walikuwa wanamkaribisha kwa heshima. Mama alipokabiliana na changamoto ya aina yoyote nyumbani alipiga simu kuwajulisha walimu mathalani katika ugonjwa, au kukosa masomo kwa sababu yoyote ile **(4)**.

Leo hii, mama R. anajiamini zaidi hususani anapozungumza na walio na mamlaka. Peke yake aliweza kumsajili mwanaye mdogo kuanza shule ya wali, na mwaka huu ameanza darasa la kwanza. Dada zake wanaendelea vizuri na sasa wako darasa la sita. Leo hii unapozungumza na mama R. furaha yake ni katika tumaini kwamba wanaye wakubwa wanatarajia kumaliza shule ya msingi mwaka ujao.

See ukurasa 4:
**(1)** Pendekezo 13
**(2)** Pendekezo 15
**(3)** Pendekezo 11
**(4)** Pendekezo 12



***Kutokana na kisa hiki cha mafanikio kuhusiana na mahudhurio ya shule ya msingi tunaweza kujifunza kitu gani?***

# "Kutokana na kisa hiki cha mafanikio kuhusiana na mahudhurio ya shule ya msingi tunaweza kujifunza kitu gani?"

Tukiangalia kisa hiki tunaona kwamba wadau wakubwa walihusika: mama, watoto, mwalimu mkuu, mwalimu wa darasa na mfanyakazi wa kujitolea wa ATD. Hii inaonesha umuhimu wa kila mmoja katika kufikia mafanikio. Kupitia kisa hiki tunaweza kuona ni wakati gani mapendekezo ya ATD ya Elimu kwa wote yanapokuwa na umuhimu zaidi. Kwa mfano:




## Pendekezo 11

**Kuwepo na mfumo wazi wa mawasiliano kati ya walimu na wazazi. Mawasiliano yanaweza kuwa kwa njia ya mikutano, simu, barua au kutembeleana.**

Mama anapopeana namba za simu na mwalimu na mwalimu mkuu na kutembelea shule mara kwa mara, inakuwa ni rahisi kufuatilia maendeleo ya watoto na hakuna tukio lingine lililotokea kusababisha watoto kufukuzwa shule.

## Pendekezo 12

**Kujenga uaminifu na kuboresha mahusiano, washikadau wote wa elimu wanapaswa kuendeleza kutambua kuheshimiana kuhusu hali za wengine.**

Kwa mama na watoto walielewa mwalimu mkuu alipoona aibu pale alipoona polisi anakuja shuleni kwake. Mwalimu wa darasa, yeye alielewa umuhimu wa kuheshimu na kusikiliza hali ya mama. Hii iliruhusu washirika wote kufanya kazi kuelekea katika lengo lao kwa pamoja na katika mazingira ya kuaminiana.

## Pendekezo 13

**Kila shule inapaswa kuwa na mfanyakazi wa kuifikia jamii ambaye jukumu lake ni kutengeneza mahusiano kati ya walimu na wazazi na kuhakikisha uwepo wa mawasiliano ya mara kwa mara haswa kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri.**

Katika kisa chetu, mfanyakazi wa kujitolea wa ATD alishika nafasi ya mfanyakazi wa jamii, akifuatana na mama na kumsaidia. Bila uwepo wa mfanyakazi wa kujitolea ATD, matokeo ya hali ya watoto hawa ingekuwaje?


## Pendekezo 15

**Kama wazazi wana malalamiko kunatakiwa kuwe na hatua wazi za kufuata na wahakikishiwe kuwa hakutakuwa na matokeo mengine kama watalalamika.**

Mama aliweza kwenda kuzungumza na mwalimu baada ya kudhalilishwa na mwalimu wa darasa, hii ilimwezesha kwenda katika hatua ya pili ambayo ilimwezesha kuwarudisha watoto wake shuleni. Endapo milango ya mwalimu mkuu isingekuwa wazi angebaki akiwa amedhalilika na kukata tamaa.

***Tangu mapendekezo ya ATD ya Elimu kwa wote yalipochapishwa kipindi cha Julyiliyopita, ulishawahi kushirikishana na jirani yako? Umewahi kujadiliana na yote katika shule anayosoma mwanao? Endapo ama mwalimu au mzazi amejaribu kutumia mapendekezo haya, iwapo jibu ni ndiyo, umeyatumiaje? Tungependa sana kupata mrejesho kutoka kwako kuhusu cho chote ulichosoma au uzoefu wako katika kujaribu kupeleka Elimu kwa Wote kwa ajili ya watoto katika jumuia yako***

***Wasiliana nasi!:***
***Hamisi Mpana: 0717308576***
***Team contact: atd.tanzania@gmail.com***




Upatikanaji Wa Elimu Ya Msingi
kwa watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri

Download: http://urlink.fr/wUZ
Order: 0717 308 576

ATD
FOURTH WORLD

STOP
POVERTY
ALL TOGETHER IN DIGNITY

## Mwito wa Kutekeleza Kampeni:
## Saini uungane na maelfu ya watu ambao wameisha weka sahihi zao.

Pamoja na matukio katika mabara matatu, Shirika la Kimataifa ATD Dunia ya Nne lilizindua kampeni yake Umaskini Basi kote duniani tarehe 12 Februari 2017 ikiwana maana ya kuwafanya wale wanaoishi katika umaskini uliokithiri kuwa washiriki katika mapambano ya kutokomeza umaskini.

“Mara nyingi watu wanaoishi katika uso wa umaskini hutumika kuleta hofu, kutoa wito wa kujengwa kuta na kuwatenga wageni”. Cassum Uteem, Rais wa ATD Dunia ya Nne na ambaye pia ni Rais mstaafu wa Mauritius alisema, “Mwaka huu 2017, tunataka kuiambia dunia juu ya mtu mmoja (Joseph Wresinski) ambaye alianzisha harakati za kuunganisha watu – walewanaoishi katika umaskini na wasiouishi – ili kuondoa vikwazo vinavyowafanya baadhi ya watu kubakia chini,

Katika kpindi cchote cha mwaka huu,tunawakaribisheni nyote kujiunga na wito wa kusema sasa Umaskini Basi. Utapendekewa kusaini, kutoa sautiyako au ushuhuda. Ulizia kwa wana ATD wengine, shirikishana na familia yako, marafiki na majirani kujiunga na wito huu. Katika mwaka huu wa mwaka 2017 pia tuliadhimisha miaka 100 ya kuzaliwa Joseph Wresinski tarehe 12 Februari (angalia ukurasa wa 8) vile vile tunayo maadhimisho ya miaka 30 ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Umaskini na miaka 60 ya kuanzishwa shirika.

Saini uungane na maelfu ya watu ambao wameisha weka sahihi zao:
**Kwa Kiingereza: http://www.atd-fourthworld.org/stop-poverty/call-to-action**
**Kwa Kiswahili: http://www.atd-fourthworld.org/stop-poverty/call-to-action/call-action-swahili/**




Mwezi Machi 2017, mjini Dakar, Senegal, ATD Dunia ya Nne kanda ya Afrika ilikaribisha wajumbe wa ATD kutoka Senegal, Afrika ya Kati, Congo DR, Cameroon, Burkina Faso, Tanzania na Ivory Cost kwa ajili ya mkutano kuu. Watu walikusanyika kwa mujibu wa utaratibu uliokubalika huko Bangui mnamo Julai 2016

Mkutano huo wa kimataifa ulikua na lengo la "*kuchukua hatua ambayo itaruhusu kila mtu kuchangia kwa kadri ya uwezo wake katika mapambano kuushinda umaskini uliokithiri:*"

***Kutokomeza umaskini kunahitaji jitihada. Kwa sababu, kila mtu ni muhimu, unahitajika mwendelezo wa kuwatafuta watu katika hatari ya kuwaacha nyuma. Inahitajika kujenga ushirikiano endelevu ambapo kila mmoja anaweza kutengeneza sauti yake ili aweze kushiriki kwa uhuru. Kwa watu waliozaliwa katika misukosuko ya mara kwa mara ya umaskini uliokithiri, pia kwa wale walioamua kushirikiana nao katika umoja, haiepukiki kwamba upo wakati ambapo ujasiri wa kusonga mbele unakosekana. Kuendelea kuboresha ujasiri wetu, tunajituma kuendeleza utashi wa pamoja ambao sote tunauhitaji ili tuweze kusonga mbele kwa pamoja. (source: http://www.atd-fourthworld.org).***

# DAKAR, Machi 2017:
# JITOLEE KWA MOYO WAKO WOTE BILA KUMUACHA MTU NYUMA

- Kusaidia wanachama wote "*kukutana na watu wengine walio na malengo ya pamoja ili kushirikiana katika kutafakari juu ya kuimarisha ushirikiano na utendaji wa majukumu katika kazi zao.*"
- "*Kujenga uhusiano zaidi kati ya wanachama wanaoshiriki kwa njia mbalimbali ili kuboresha uwezo wa kufanya kazi, pamoja na kusaidiana katika mazingira mbalimbali.*"

Huko Dakar, wakati wa duru ya mazungumzo ya wanachama, wasomi na watu kutoka makundi mbalimbali, Vamara, rafiki kutoka Ivory Coast alisema, *'Ninapenda kufanya kazi na watu wengine katika kupambana dhidi ya umasikini sihitaji kuwa na furaha peke yangu'.*

Baada ya Dakar, mchakato huo utafuata hapa nchini Tanzania, Dar Es Salaam na nje ya Dar Es Salaam, ili kufikiri ni jinsi gani wanachama watashiriki kuwajibika kwa Muungano.

## MAHOJIANO

> ***"Moja wapo ya jukumu letu ni kuwasilisha maneno ya wale wanaoishi katika maisha magumu zaidi bila kubadili maana yake."***

Alexia Gasengayire, Venance Magombera na Reuben Mtitu walikwenda Dakar kuwakilisha ATD Dunia ya Nne Tanzania wakibeba sauti za wanachama wake. Kupitia kujitoa kwao, kila mmoja alirejea na uzoefu wake. Alexia, mfanyakazi wa kudumu wa shirika, Venance ambaye amejitoa kikamilifu kwa ajili ya jirani zake yeye mwenyewe akiwa mzoefu katika umaskini uliokithiri, Reuben akieneza ujumbe na malengo ya shirika kupitia ushirika wake Njombe.

Tuliwaomba Alexia na Venance kushirikishana nasi uzoefu wao katika maisha waliyoishi kule kwa wiki nzima.

**Venance**: Inabidi niseme kwamba majuma machache kabla ya safari nilijihisi kuwa katika mashaka. Miezi michache kabla, mimi na wenzangu tulikuwa tumependekezwa kuhudhuria katika mkutano huo. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kushiriki katika mkutano wa kimataifa na nilifurahi sana kupata fursa ya kujifunza kutoka kwa wenzangu kutoka Afrika. tulikuwa tumerithi kazi iliyokuwa imefanyika kule Bangui mwaka 2016 ambayo ilifungua maswali mengi kuhusu kushirikishana majukumu katika kujitoa kwetu. Nilikuwa na mashaka endapo nitaweza kuwakilisha kile nilichokuwa nimejifunza Tanzania. Hakika lilikuwa jukumu kubwa mno.

**Alexia**: Mara tulipowasilil, tulijiunga na kikundi, tulijisikia katika umoja imara kati yetu licha ya tofauti zetu, tukitoka katika nchi tofauti. Tulijisikia kuwa na nguvu.

**Venance**: Hata kama tulikuwa hatufahamiani, mara tulijiona wamoja kama vile tulikuwa tunafahamiana kwa muda mrefu, kwa urafiki uliojitokeza hatukuona tofauti zetu. Tulipowasili hatukujisikia kuchoka, tulipata nguvu sana. Huu ndio moyo wa ATD.

**Alexia**: Haraka tuliweza kushirikishana maswali yetu. Wengine walifafanua ilivyokuwa vigumu wakati mwingine kuwatembelea walio katika umaskini uliokithiri bila kitu mifukoni mwetu zaidi tu ya muda wetu, urafiki wetu, utashi wetu wa kujifunzana kuelewa. Wengine walijibu kwamba kwa wale walioachwa nyuma, kukaribisha marafiki ni kitu cha thamani mno kwao, msaada mkubwa ambao hauwezi kulinganishwa na chochote.

**Venance**: Kitu kimoja cha muhimu, tunachojaribu kushirikishana na kujenga katika kushirikishana majukumu, tulikifanya kwa vitendo katika wiki ile yote. Kushirikishana katika kuzungumza, kuchukua majukumu tofauti katika wiki nzima n.k.

**Alexia**: Kama matokeo ya mabadilishano haya, tuliona kwamba kila mmoja anao wajibu wa kufanya. Jukumu katika shirika ni kitu cha kushirikishana. Wanachama hawahitaji kuwa wafanyakazi wa kudumu katika shirika ndipo waweze kutekeleza majukumu yao.

**Venance**: Moja wapo ya jukumu letu ni kuwasilisha maneno ya wale wanaoishi katika maisha magumu zaidi kwa uaminifu bila kubadili maana yake.



Alexia Gasengayire, Reuben Mtitu, Venance Magombera



Duru ya majadiliano mezani




Fatoumata (Burkina Faso)

## *Siku maalumu ya kuadhimmisha miaka 100 ya kuzaliwa Joseph Wresinski, muasisi wa ATD Dunia ya Nne.*

Tarehe 12 ya Februari 2017 ilikuwa siku maalumu sana kwa sababu kadhaa.Kila mahali duniani shirika liliadhimimsha kumbukumbu mmoja ambaye alipata uzoefu wa umaskini uliokithiri utotoni mwake. Njaa, kudhalilishwa,na akabeba sauti za hao wanaoishi maisha hayo hadi mahali, katika taasisi ambazo masuala ya dunia huamuliwa. Ofisi ya ATD Mwananyamala ilifungua ofisi zake kwa takribani rafiki 50 wa shirika kuadhimisha pamoja tarehe hiyo. Washa kadhaa ziliratibiwakuwawezesha washiriki kuifahamu mizizi ya ATD, maisha ya muasisi wake na historia ya ATD Tanzania: Hazi hapa picha za siku hiyo.



Semina ya historia ya ATD Dunia ya Nne Tanzania kwa picha.



Semina ya mapitio ya vitendo vya ATD Dunia ya nne Tanzania



Mama Maria na Selemani walitoa mitazamo yao baada ya kutazama filamu ya historia ya miaka 50 ya Joseph Wresinski.



Reuben anatambulisha na kushirikisha dhamira aliyonayo na jinsi atakavyoitekeleza akiwa Njombe.









Semina ya maisha ya utoto ya Joseph Wresinski diaporama.



Kundi la vijana la mchezo wa kuigiza.



Uwasilishwaji wa filamu ya miaka 50 ya Joseph Wresinski



Hitoria ya makazi duni ya Noisy-le-Grand (mahali ambapo ATD Dunia ya nne ilizaliwa).

**Wasiliana nasi!**

ATD Fourth World - P.O. Box 61786 - Dar es Salaam
Office number: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
English website : http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/
Kiswahili website : http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/
**Facebook page**: https://www.facebook.com/atd.duniayanne